



Australian Government

Department of Home Affairs

Shauri kwa kutumia Wakala wa Uhamiaji Aliyeandikishwa

OMARA ni nini?

OMARA (Office of the Migration Agents Registration Authority) ni sehemu ya idara ya uhamiaji, yaani Department of Home Affairs (the Department). OMARA ni shirika lenye kanuni ambalo linahakikisha watu wazuri na wenye kufaa na wanakubaliwa kuwa mawakala wa uhamiaji walioandikishwa na inachunguza malalamiko dhidi ya mawakala.

Kuchagua wakala wa uhamiaji

- Mawakala wote wa uhamiaji walioandikishwa wana Namba ya Usajili wa Mawakala wa Uhamiaji ya kipekee, au MARN (*Migration Agents Registration Number*).
- Unaweza kuangalia kama mtu ameandikishwa kwa kutafuta kwa MARN yake kwa tovuti ya OMARA.
- **Hakuna mtu anayeweza kuahidi utapata viza – hata kama mtu ni wakala wa uhamiaji aliyeandikishwa.**
- Isipokuwa msamaha, sio halali kwa mtu yeyote kutoa ushauri wa uhamiaji nchini Australia kama hakuandikishwa na OMARA. Orodha ya watu wanao usamaha inaweza kugunduliwa kwenye Fomu ya 956.

Shauri na madokezo unapotumia wakala wa uhamiaji

Wakala wako afanye:

- akupatie nakala ya Mwongozo wa Mtumiaji (*Consumer Guide*) mara moja amekubalia kufanya shughuli kwa ajili yako. Unaweza pia kupata nakala kutoka tovuti ya OMARA.
- akupatie *Maelezo ya Huduma (Statement of Services)* yanayorodhesha huduma atakazokugharamia kubla hujalipa.
- rudisha hati zozote zinazokuwa zako katika siku 7 baada ya umeziomba.
- tunza kumbukumbu ya mawasiliano yote kuhusu ombi lako nawe na ya the Department.

Ufanye:

- tunza hati zako za asili kama paspoti na vyeti vyako vya kuzaliwa. Hati nyingi the Department inazohitaji zinaweza kutolewa kama nakala halali.

- Hakikisha mazungumzo yote na maelekezo yote yako kwa wakala wako kwa maandishi. Una majukumu kwa maelezo yanayotolewa kwa the Department – hata kama mtu mwingine amejaza fomu.
- Elewa huduma gani ni pamoja na kama sehemu ya ada ya wakala. Orodha ya ada wastani za wakala inaweza kugunduliwa kwa tovuti ya OMARA.

Maswala kuhusu wakala wako wa uhamiaji

- Wasiliana na OMARA ikiwa unahitaji ushauri.
- **Kutoa lalamiko hataathiri ombi lako la viza.**
- Watu ambao hawakuandikishwa na wanatoa ushauri wa uhamiaji nchini Australia wapigiwa ripoti kwa Idara kwenye namba ya 1800 009 623.
- likwa hutaki tena kushughulikia na wakala wako wa uhamiaji, ufahamishe the Department kwa njia ya kujaza Sehemu B & C ya Fomu 956.

Angalia kama mtu ameandikishwa kwenye www.mara.gov.au:

The screenshot shows a search interface titled "Search for an agent". It features a map with location pins and a "Search map" button. Below the map, there are two input fields: "Location" with a placeholder "eg. country, state, city, town, suburb, postcode" and "Agent" with a placeholder "eg. agent's family name or MARN". A blue "Search" button is positioned below these fields. At the bottom, there are links for "More search options" and "Clear".

Maelezo zaidi

Office of the Migration Agents Registration Authority:
www.mara.gov.au au Simu: 1300 226 272

Department of Home Affairs:
www.homeaffairs.gov.au au Simu: 131 881

Kuongea na mtafsiri pigia simu Huduma ya Utafiti na Ukalimani (TIS) kwenye 131 450.